request the local program to correct the information.	programu ya ndani kuzisahihisha taarifa hizo.
Page 18	Page 18
The local program must decide whether to correct the information within a reasonable period of time after receiving the request. If the program refuses to correct the information as you request, you must be informed of the refusal in writing and be told of the right to a hearing.	Lazima programu ya ndani iamue ikiwa itasahihisha taarifa hizo ndani ya kipindi kinachofaa baada ya kupokea ombi. Ikiwa programu inakataa kusahihisha taarifa hizo kama unavyoomba, lazima ufahamishwe kuhusu sababu ya kukataa kwa njia ya maandishi na uambiwe kuhusu haki ya usikilizwaji.
The local program, on request, must provide an opportunity for a hearing to challenge information in early intervention records to ensure that it is accurate, not misleading, or otherwise in violation of the privacy or other rights of the child or parent(s).	Lazima programu ya ndani itoe fursa ya usikilizwaji ili kupinga taarifa zilizo katika rekodi za mikakati ya mapema unapooomba ili kuhakikisha kwamba ni sahihi, hazipotoshi, au vinginevyo hazikiuki faragha wala haki nyingine za mtoto au wazazi.
If, as a result of a hearing, the local program decides that the information is inaccurate, misleading, or otherwise in violation of the privacy or other rights of the child or parent, the local program must amend the information accordingly and inform the parent in writing.	Ikiwa, kutokana na usikilizwaji, programu itaamua kwamba taarifa si sahihi, zinapotosha au vinginevyo zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto au mzazi, lazima programu ya ndani irekebishe taarifa ipasavyo na kumfahamisha mzazi kwa njia ya maandishi.
If, as a result of a hearing, the local program decides that the information is accurate, not misleading, or not in violation of the privacy or other rights of the child or parent, you must be informed of your parent's right to place a statement commenting on the information or setting forth any reasons for disagreeing with the decision of the local program, in the early intervention record.	Ikiwa, kutokana na usikilizwaji, programu ya ndani itaamua kwamba taarifa ni sahihi, hazipotoshi wala kukiuka faragha au haki nyingine za mtoto au mzazi, lazima ufahamishwe kuhusu haki yako ya mzazi ya kutoa taarifa yenye maoni kuhusu taarifa au kutoa sababu yoyote ya kupinga uamuzi wa programu ya ndani, katika rekodi ya mikakati ya mapema.
Any explanation placed in the records of your child under these procedures must:	Ufafanuzi wowote uliowekwa katika rekodi za mtoto wako kwa mujibu wa taratibu hizi lazima:
• Be maintained by the local program as part of the early intervention records of your child as long as the record is maintained by such program. If the early intervention records of your child or the	• Udimishwe na programu ya ndani kama sehemu ya rekodi za mikakati ya mapema za mtoto wako mradi tu rekodi inadumishwa na programu hiyo. Ikiwa rekodi za mikakati ya mapema za mtoto

parts you disagree with are disclosed by the local program to any party, the explanation must also be disclosed to the party.	wako au sehemu unazopinga zilifichuliwa na programu ya ndani kwa mhusika yeyote, lazima ufafanuzi pia ufichuliwe kwa mhusika.
A hearing held under this section must be conducted according to the procedures under the Family Education Rights and Privacy Act (FERPA) regulations at 34 CFR § 99.22 and Kansas Administrative Regulations.	Usikilizwaji uliofanyika kwa mujibu wa sehemu hii lazima ufanywe kulingana na taratibu kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya Haki za Elimu na Faragha ya Familia (FERPA) kwenye 34 CFR § 99.22 na Kansas Administrative Regulations.
Page 19	Page 19
Confidentiality 34 CFR § 303.401, 303.402	Usiri 34 CFR § 303.401, 303.402
Personally identifiable means the information including:	Kutambulisha mtu binafsi inamaanisha taarifa ikiwa ni pamoja na:
• The name of your child, parent or other family member. • The address of your child. • A personal identifier such as the child's or parents' social security number; and • A list of personal characteristics or other information that would make it possible to identify the child with reasonable certainty.	• Jina la mtoto wako, mzazi, au mwanafamilia mwengine. • Anwani ya mtoto wako. • Kitambulisho cha binafsi kama vile nambari ya ruzuku ya serikali ya mtoto au wazazi; na • Orodha ya sifa za mtu au taarifa nyingine ambazo zitawezesha kumtambua mtoto kwa uhakika unaofaa.
Parental consent must be obtained before personally identifiable information is:	Lazima idhini ya mzazi ichukuliwe kabla ya taarifa zinazomtambulisha mtu binafsi:
• Disclosed to anyone other than authorized representatives, officials or employees of the local program in collecting, maintaining or using information under Part C, unless it is Part C information contained in the record and is authorized under FERPA (34 CFR § 99.31); and/or used for any purpose other than meeting a requirement under Part C.	• Hazijafichuliwa kwa mtu yeyote ambaye si wawakilishi walioidhinishwa, maafisa au waajiriwa wa programu ya ndani katika kukusanya, kudumisha au kutumia taarifa kwa mujibu wa Sehemu ya C, isipokuwa ni sehemu ya taarifa za Sehemu ya C zilizo katika rekodi na zimeidhinishwa kwa mujibu wa FERPA (34 CFR § 99.31); na/au zilizotumiwa kwa madhumuni yoyote ambayo si kukidhi mahitaji kwa mujibu wa Sehemu ya C.
Page 20	Page 20
In accordance with CFR § 303.401 (d), the local program must share to the Local Educational Agency and the State	Kwa mujibu wa CFR § 303.401 (d), lazima programu ya ndani ishiriki kwa Shirika la Elimu la Ndani na Shirika la Elimu la Jimbo

Educational Agency the following: child's name, child's date of birth and parent contact information. This includes name, address and telephone number. The purpose of sharing is in order to meet the requirement to identify all potentially eligible children and does not require parental consent.	maelezo yafuatayo: jina la mtoto, tarehe ya mtoto ya kuzaliwa na maelezo ya mawasiliano ya mzazi. Hii ni pamoja na jina, anwani na nambari ya simu. Madhumuni ya kushiriki ni kwa ajili ya kukidhi mahitaji ili kutambua watoto wote wanaoweza kustahiki na hayahitaji idhini ya mzazi.
The following safeguards must be in place to ensure and protect confidentiality of records:	Lazima ulinzi ufuatao uwepo ili kuhakikisha na kulinda siri ya rekodi:
• Each local program must protect the confidentiality of personally identifiable information at collection, maintenance, use, storage, disclosure, or destruction stages. • The coordinator of each local program is the one responsible for ensuring the confidentiality of any personally identifiable information. • All persons collecting or using personally identifiable information must receive training or instruction regarding Kansas' Part C policies and procedures which comply with IDEA and FERPA (34 CFR § 99.3). • Each local program must maintain, for public inspection, a current listing of the names and positions of those employees within the agency who have access to personally identifiable information. • The local program must inform parents when personally identifiable information collected, maintained, or used under Part C is no longer needed to provide services to the child or family. • The information must be destroyed at the request of the parents. (Permanent records of your child's name, date of birth, parent	• Lazima kila programu ilinde siri ya taarifa zinazomtambulisha mtu binafsi kwenye hatua za ukusanyaji, udhumishaji, matumizi, uhifadhi, ufichuaji au uharibifu. • Mratibu wa kila programu ya ndani ndiye aliye na jukumu la kuhakikisha siri ya taarifa yoyote inayomtambulisha mtu binafsi. • Watu wote wanaokusanya au kutumia taarifa zinazomtambulisha mtu binafsi lazima wapate mafunzo au maagizo kuhusu sera na taratibu za Sehemu ya C za Kansas ambazo zinatii IDEA na FERPA (34 CFR § 99.3). • Kila programu ya ndani lazime idumishe orodha ya sasa ya majina na maelezo ya waajiriwa ambao wamo ndani ya shirika walio na idhini ya kufikia taarifa zinazomtambulisha mtu binafsi kwa ajili ya uchunguzi wa umma. • Lazima programu ya ndani iwafahamishe wazazi wakati taarifa zinazomtambulisha mtu binafsi zimekusanywa, kudumishwa au kutumiwa kwa mujibu wa Sehemu ya C hazihitajiki tena ili kutoa huduma kwa mtoto au familia. • Lazima taarifa ziharibiwe kwa ombi la wazazi. (Rekodi za kudumu zenye jina,

contact information, address, phone number, enrollment date and completion date, may be maintained without time limitations.) • Local programs must give notice to fully inform parents about confidentiality of personally identifiable information.	tarehe ya kuzaliwa ya mtoto wako, taarifa za mawasiliano ya mzazi, anwani, nambari ya simu, tarehe ya uandikishaji na tarehe ya kukamilisha, zinaweza kudumishwa bila vikomo vya muda.) • Lazima programu za ndani zitoie notisi ili kuwafahamisha wazazi kikamilifu kuhusu siri ya taarifa zinazomtambulisha mtu binafsi.
Page 21	Page 21
Dispute Resolution 34 CFR § 303.430	Suluhisho la Migororo 34 CFR § 303.430
Kansas Dispute Resolution Options	Machaguo ya Utatuzi wa Migogoro ya Kansas
We encourage you to resolve any disagreements with your local program staff. If you disagree with a local program on the identification, evaluation, placement of your child, or provision of appropriate early intervention services to your child or family, KDHE has procedures in place to address your concerns. These concerns may be addressed by:	Tunakuhimiza usuluhishe pingamizi yoyote na mfanyakazi wako wa programu ya ndani. Ikiwa hukubali programu ya ndani kuhusu utambulisho, tathmini, kumweka mtoto wako katika makao ya utunzaji, au utoaji wa huduma zinazofaa za mikakati ya mapema kwa mtoto au familia yako, KDHE ina taratibu za kushughulikia wasiwasi wako. Wasiwasi huu unaweza kuangaziwa kwa:
1. Informal Complaint: an informal way to address matters of concern that are resolved within 10 to 15 business days. 2. Formal Complaint: a formal, written complaint to KDHE which is resolved within 60 calendar days. 3. Mediation: a meeting with a neutral person (a mediator) to talk about the problem and try to produce a solution that is acceptable to both parties. 4. Due Process Hearing: a formal process with a neutral person (a hearing officer) who listens to the party filing the complaint and to the parties involved to	5. Malalamishi Yasiyo Rasmi: njia isiyo rasmi ya kuangazia masuala ya wasiwasi yanayosuluhishwa ndani ya siku 10 hadi 15 za kazi. 6. Malalamishi Rasmi: malalamishi rasmi yaliyoandikwa kwa KDHE ambayo yanasuluhishwa ndani ya siku 60. 7. Upatanishi: mkutano na mtu asiyeegemea upande wowote (mpatanishi) ili kuzungumza kuhusu tatizo na kujaribu kupata suluhisho linalokubalika kwa wahusika wote wawili. 8. Usikilizwaji wa Mchakato Unaofaa: mchakato rasmi na mtu asiyeegemea upande wowote (afisa wa usikilizaji)

decide who is right and how to resolve the problem.	anayesikiliza mhusika anayewasilisha malalamishi na kwa wahusika wanaohusika katika kuamua aliye sahihi na jinsi ya kutatua tatizo.
Forms may be accessed on KECDS website at kdhe.ks.gov/677 , requested by calling (785) 296-3319 or by emailing KDHE.KECDS@ks.gov . A request for mediation or due process may be requested at the same time that a formal complaint is made.	Fomu zinaweza kupatikana kwenye tovuti ya KECDS kwenye kdhe.ks.gov/677 , zilizoombwa kwa kupiga simu (785) 296-3319 au kwa kutuma barua KDHE.KECDS@ks.gov . Ombi la upatanishi au mchakato unaofaa linaweza kuombwa wakati mmoja na malalamishi rasmi yanapotolewa.
Page 22	Page 22
Complaints 34 CFR § 303.433, 434	Malalamishi 34 CFR § 303.433, 434
An informal complaint is available by calling KDHE at (785) 296-3319.	Malalamishi rasmi yanapatikana kwa kupigia simu KDHE kwa nambari (785) 296-3319.
A formal complaint can be filed by an individual or organization, including those from another state. The complaint process includes submitting a written signed complaint against KDHE, KECDS, or any local program that is violating a requirement of the Part C program.	Malalamishi rasmi yanaweza kuwasilishwa na mtu au shirika, ikiwa ni pamoja na wale wanaotoka kwenye jimbo jingine. Ikiwa mchakato wa malalamishi ni pamoja na kuwasilisha malalamishi ya maandishi yaliyotiwa sahihi dhidi ya KDHE, KECDS, au programu yoyote ya ndani inayokiuka mahitaji ya programu ya Sehemu ya C.
The complaint must include:	Lazima malalamishi yawe pamoja na:
• A statement that a requirement of Part C has been violated by KECDS, a local program or a local provider. • A statement of the facts on which the complaint is based; and • The contact information and signature of the person filing the complaint.	• Taarifa kwamba mahitaji ya Sehemu ya C yamekiukwa na KECDS, programu ya ndani au mtoa huduma wa ndani. • Taarifa ya mambo ya uhalisia ambayo malalamishi yametokana nayo; na • Maelezo ya mawasiliano na sahihi ya mtu anayewasilisha malalamishi.
If alleging violations in respect to a specific child, the name and residence of that child, the name of the local program and the provider(s) serving the child, a description of the nature of the problem of the child, including facts relating to the	Ikiwa unadai ukiukaji kuhusiana na mtoto mahususi, jina na makazi ya mtoto huyo, jina la programu ya ndani na mtoa huduma anayemhudumia mtoto, maelezo ya hali ya tatizo la mtoto, ikiwa ni pamoja na mambo ya uhalisia yanayohusiana na tatizo la

problem of the child, and a proposed resolution to the extent known and available to the party at the time the complaint is filed, must be included in the complaint.	mtoto na suluhisho linalopendekezwa kwa kiasi kinachojulikana na kupatikana kwa mhusika wakati malalamishi yanapowasilishwa, lazima yajumuishwe katika malalamishi.
A copy of the complaint must be sent to the local program/provider(s) at the same time the complaint is filed with KDHE.	Nakala ya malalamishi lazima itumwe kwa programu/mtoa huduma wa ndani kwa wakati mmoja na malalamishi yanapowasilishwa kwa KDHE.
What happens after I file a formal complaint?	Je, ni nini kinachotokea baada ya kuwasilisha malalamishi rasmi?
Remember that continued communication between parents and professionals at all stages is important. It will help to ensure resolution of complaints in a satisfactory manner.	Kumbuka kwamba mawasiliano ya mara kwa mara kati ya wazazi na wataalamu kwenye hatua zote ni muhimu. Yatasaidia kuhakikisha suluhisho la malalamishi kwa njia ya kuridhisha.
• You will be sent information about your rights. • You will be informed of the next steps that need to be taken. • You will have a chance to have questions answered.	• Utatumiwa taarifa kuhusu haki zako. • Utafahamishwa kuhusu hatua zinazofuata zinazohitaji kuchukuliwa. • Utapata nafasi ya maswali kujibiwa.
Page 23	Page 23
• The process will be monitored by Kansas Early Childhood Developmental Services. • Kansas Early Childhood Developmental Services will follow up after resolution has been reached to make sure that all agreements are fulfilled. • Your child will continue to receive services that are not in dispute.	• Mchakato utafuatiliwa na Kansas Early Childhood Developmental Services. • Kansas Early Childhood Developmental Services itafuatilia baada ya suluhisho kupatikana ili kuhakikisha kwamba makubaliano yote yanatimizwa. • Mtoto wako ataendelea kupokea huduma ambazo hazina pingamizi.
Formal complaints must be filed and received by KDHE within one (1) year of the alleged violation. Once KDHE has received the complaint, it has sixty (60) days to:	Lazima malalamishi rasmi yawasilishwe na kupokelewa na KDHE ndani ya mwaka mmoja (1) wa ukiukaji unaodaiwa. Pindi KDHE inapopokea malalamishi, ina siku sitini (60) za:
• Investigate the complaint, including conducting an independent, on-site investigation, if necessary.	• Kuchunguza malalamishi, ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa kituoni ambao

• Allow the local program to respond to the complaint, including a proposal to resolve the complaint. • Make an independent determination as to whether or not a violation of a Part C requirement has occurred after reviewing all relevant information. • Issue a written decision to the complainant that addresses each allegation in the complaint and that contains the facts and conclusions as well as the reasons for the final decision.	ni huru, ikihitajika. • Kuruhusu programu ya ndani kujibu malalamishi ikiwa ni pamoja na pendekezo la kusuluhisha malalamishi. • Kufanya uamuzi huru wa ikiwa ukiukaji wa mahitaji ya Sehemu ya C yametokea au hayajatokea baada ya kukagua taarifa zote husika. • Kumpa mlalamishi uamuzi wa maandishi unaoangazia kila dai katika malalamishi na ulio na mambo ya uhalisia na mahitimisho na pia sababu za uamuzi huo wa mwisho.
Page 24	Page 24
Timelines may be extended if there are exceptional circumstances with respect to a particular case or if the parties have agreed to extend the timelines to engage in mediation.	Muda unaweza kuongezwa ikiwa kuna hali za kipekee kuhusiana na kesi husika au ikiwa wahusika wamekubaliana kuongeza muda ili kushiriki katika mapatano.
Procedures for effective implementation of KDHE's final decision will include technical assistance activities, negotiations and corrective actions to achieve compliance.	Taratibu za utekelezaji bora wa uamuzi wa mwisho wa KDHE zitakuwa ni pamoja na shughuli za usaidizi wa kiufundi, makubaliano na hatua za urekebishaji ili kufanikisha utii.
The individual or organization filing the complaint has the opportunity to submit additional information, either orally or in writing, about the complaint. If the final decision indicates that appropriate services were not/are not being provided, KDHE must address:	Mtu au shirika linalowasilisha malalamishi lina fursa ya kuwasilisha taarifa za ziada, kwa njia ya mdomo au ya maandishi, kuhusu malalamishi. Ikiwa uamuzi wa mwisho unaonyesha kwamba huduma zinazofaa hazikutolewa/hazitolewi, lazima KDHE inangazie:
• How to correct the denial of those services including, as appropriate, the awarding of monetary reimbursement or other corrective action appropriate to the needs of the child and the child's family; and • Appropriate future provision of services for all infants and toddlers with disabilities and their families.	• Jinsi ya kusahihisha kunyimwa kwa huduma hizo ikiwa ni pamoja na, inavyofaa, utoaji wa fidia ya pesa au hatua nyingine ya urekebishaji inayofaa mahitaji ya mtoto na familia ya mtoto; na • Utoaji wa huduma zinazofaa za siku zijazo kwa watoto wachanga na wanaodema walio na ulemavu na familia zao.

If a formal written complaint is received that is also the subject of a due process hearing, or contains multiple issues, of which one or more are part of that hearing, KDHE must set aside any part of the complaint that is being addressed in the due process hearing until the conclusion of the hearing. Any issue in the complaint that is not a part of the due process action must be resolved within the 60 calendar day timeline using the complaint procedure described above.	Ikiwa malalamishi rasmi ya maandishi yanapokelewa ambapo pia yanazingatia usikilizwaji wa mchakato unaofaa, au yana matatizo mengi, ambayo moja au zaidi ni sehemu ya usikilizwaji huo, lazima KDHE iweke kando sehemu yoyote ya malalamishi yanayoangaziwa katika usikilizwaji wa mchakato unaofaa hadi hitimisho la usikilizwaji. Tatizo lolote lililo katika malalamishi ambalo si sehemu ya mchakato unaofaa lazima litatuliwe ndani ya siku 60 kwa kutumia utaratibu wa malalamishi ulioelezwa hapo juu.
Complaints that have already been decided in an impartial due process hearing involving the same parties cannot be considered under this procedure. KDHE must notify the complainant that the hearing decision is binding. Any complaint alleging that an agency failed to implement a due process hearing must be resolved by KDHE.	Malalamishi ambayo tayari yameamuliwa katika usikilizwaji wa mchakato unaofaa usiopendelea upande wowote unaohusisha wahusika walewale hauwezi kutiliwa maanani kwa mujibu wa utaratibu huu. Lazima KDHE imwarifu mlalamishi kwamba uamuzi wa usikilizwaji unabana kisheria. Malalamishi yoyote yanayodai kwamba shirika lilishindwa kutekeleza usikilizwaji wa mchakato unaofaa lazima yasuluhishwe na KDHE.
Any party aggrieved by the findings and decision issued by a due process hearing officer has a right to file a civil action in State or Federal Court.	Mhusika yeyote aliyedhulumiwa na maamuzi haya yaliyotolewa na afisa wa usikilizaji wa mchakato unaofaa ana haki ya kuwasilisha hatua ya umma katika Mahakama ya Jimbo au Serikali Kuu.
Page 25	Page 25
Mediation 34 CFR § 303.431	Mapatano 34 CFR § 303.431
Mediation is a meeting designed to provide an opportunity to resolve a disagreement regarding Part C services and is voluntary on the part of both parties. Mediation can be requested by either individuals or organizations by submitting the form at the end of this section.	Mapatano ni mkutano uliokusudiwa kutoa fursa ya kusuluhisha pinganmizi kuhusu huduma za Sehemu ya C na ni wa hiari kwa upande wa wahusika wote wawili. Mapatano yanaweza kuombwa na mtu au shirika lolote kwa kuwasilisha fomu mwishoni mwa sehemu hii.
Mediation involves a meeting with a neutral person (a mediator) to talk about the issues and produce a solution that is acceptable to all parties. The mediator is:	Mapatano yanahusisha mkutano na mtu asiyeegemea upande wowote (mpatanishi) ili kuzungumza kuhusu matatizo na kupata

	suluhisho linalokubalika kwa wahusika wote. Mpatanishi ni: • Mtu asiyeegemea upande wowote, kunaamisha kwamba si mwajiriwa wa shirika linalotoa huduma kwa mtoto na hana nia nyingine za binafsi wala kitaalamu zinazoweza kukinzana na shabaha yake. (Mtu ambaye ana sifa za kuwa mpatanishi hachukuliwi kuwa mwajiriwa pekee kwa sababu analipwa ili kutumika kama mpatanishi.) • Mtu aliye na sifa zinazofaa ambaye amepata mafunzo ya mbinu za mapatano. • Aliye na maarifa ya sheria na kanuni zinazohusiana na utoaji wa huduma za mikakati ya mapema. • Anapewa jukumu kwa msingi wa kubahatisha, wa zamu au msingi mwingine usio wa kuegemea upande wowote. • Mapatano yataratibu mkutano ndani ya siku saba (7) baada ya kupokea ombi (lililotumwa kwa KECDS huko KDHE) lenye makubaliano ya maandishi yanayotolewa ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupokea ombi. (Ikiwa usikilizwaji wa mchakato unaofaa unaendelea, muda wa kukamilisha mapatano utakuwa siku 15 ili kuruhusu muda wa kutosha kwa ajili ya usikilizwaji kutimiza muda unaohitajika). Muda unaweza kuongezwa baada ya makubaliano na wahusika wote wawili.
Page 26	Page 26
Other things to remember about mediation:	Mambo mengine ya kukumbuka kuhusu mapatano:
• Is voluntary and must be agreed upon by both parties. • It does not interrupt (delay or deny) any of your services or rights in the program	• Ni ya hiari na lazima wahusika wote wawili wakubaliane. • Hausimamishi (kuchelewesha au kunyima) huduma au haki yako yoyote

including your right to a due process hearing. • Will be paid for by KDHE. • Will be held at a location that is convenient to both parties.	katika programu ikiwa ni pamoja na haki ya usikilizwaji wa mchakato unaofaa. • Yatalipwa na KDHE. • Yatafanywa kwenye eneo ambalo ni karibu na wahusika wote wawili.
Discussions that occur during the mediation process must be confidential and may not be used as evidence in any subsequent impartial due process hearings or civil proceedings. The parties will be allowed to sign a confidentiality pledge prior to beginning the process.	Majadiliano yanayotokea wakati wa mchakato wa mapatano lazima yawe ya siri na yasitumiwe kama ushahidi katika usikilizwaji wowote unaofuata wa mchakato unaofaa usioegemea upande wowote au kesi za kiraia. Wahusika wataruhusiwa ili kutia sahihi ahadi ya usiri kabla ya kuanza mchakato.
At the conclusion of the mediation process, both parties must sign a mediation agreement and are given a copy of the written agreement (or disagreement) that resulted from the mediation process. Any signed agreement is legally binding and enforceable in any State court of competent jurisdiction or in a district court of the United States 34 CFR § 303.431 (b) (6).	Wakati wa hitimisho la mchakato wa mapatano, lazima wahusika wote wawili watie sahihi makubaliano ya mapatano na wanapewa nakala ya makubaliano yaliyoandikwa (au pingamizi) yaliyotokana na mchakato wa mapatano. Makubaliano yoyote yaliyotiwa sahihi yanabana kisheria na kutekelezwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka au katika mahakama ya wilaya ya Marekani 34 CFR § 303.431 (b) (6).
Mediation does not restrict you from requesting a due process hearing. You may request both mediation and a due process hearing at the same time.	Mapatano hayakuwekei vikwazo vya kuomba usikilizwaji wa mchakato unaofaa. Unaweza kuomba mapatano na usikilizwaji wa mchakato unaofaa kwa wakati mmoja.
Page 27	Page 27
Due Process 34 CFR § 303.435-438	Mchakato Unaofaa 34 CFR § 303.435-438
An impartial due process hearing is a formal procedure conducted by an impartial hearing officer and is an option for families seeking to file a complaint regarding the decision of a local provider or KDHE to initiate, or change the identification, evaluation, or placement of an infant or toddler, or a change in services for that infant or toddler.	Usikilizwaji wa mchakato unaofaa usioegemea upande wowote ni utaratibu rasmi unaoendeshwa na afisa wa usikilizwaji kesi asiyeegemea upande wowote na ni chaguo kwa familia zinazotaka kuwasilisha malalamishi kuhusu uamuzi wa mtoa huduma wa ndani au KDHE ili kuanzisha, au kubadilishaa utambulisho, tathmini, au kumhamishia mtoto kwenye makao ya utunzaji, au

	kumbadilishia huduma mtoto huyo mchanga au anayedema.
Families seeking a due process hearing may submit a request by using the forms available on our website at kdhe.ks.gov/677 , requested by calling (785) 296-3319 or by emailing KDHE.KECDS@ks.gov . The request must be mailed to:	Familia zinazotaka usikilizwaji wa mchakato unaofaa zinaweza kuwasilisha ombi kwa kutumia fomu zilizopo kwenye tovuti yetu katika kdhe.ks.gov/677 , zilizombwa kwa kupiga simu (785) 296-3319 au kwa kutuma barua pepe KDHE.KECDS@ks.gov . Lazima ombi litumwe kwa:
Attn: Part C Coordinator Kansas Early Childhood Developmental Services 1000 SW Jackson, Suite 220 Topeka, Kansas 66612-1274	Attn: Part C Coordinator Kansas Early Childhood Developmental Services 1000 SW Jackson, Suite 220 Topeka, Kansas 66612-1274
The impartial due process hearing must be completed, and a written decision made, within thirty (30) calendar days' of KDHE'S receipt of the request. (Mediation, if attempted, must occur within the same 30 days.)	Lazima usikilizwaji wa mchakato unaofaa usioegemea upande wowote ukamilishwe na uamuzi wa maandishi kutolewa ndani ya siku thelathini (30) za KDHE kupokea ombi. (Ikiwa umejaribu mapatano, lazima yatokee ndani ya siku zilezile 30.)
Impartial hearing officers are appointed to conduct due process hearings. Hearing officers must have knowledge about the provisions of Part C and the needs of early intervention services available for infants and toddlers and their families. Hearing officers shall not:	Maafisa wa usikilizwaji asiyeegemea upande wowote wanateuliwa ili kuendesha usikilizwaji wa mchakato unaofaa. Lazima maafisa wa usikilizwaji wawe na maaarifa kuhusu vipengele vya Sehemu ya C na mahitaji ya huduma za mikakati ya mapema yapatikane kwa watoto wachanga na wanaodema na familia zao. Maafisa wa usikilizwaji:
• Be an employee of, or entity involved in the provision of early intervention services or care of the child. • Be an employee of KDHE because the person is paid by the agency to implement the complaint resolution process.	• Hatakuwa mwajiriwa, au shirika linalohusika katika utoaji wa huduma za mikakati ya mapema wala kumtunza mtoto. • Hatakuwa mwajiriwa wa KDHE kwa sababu mtu analipwa na shirika ili kutekeleza mchakato wa suluhisho la malalamishi.
Page 28	Page 28
• Hold a personal or professional interest that would conflict with their objectivity in implementing the process.	• Hatakuwa na nia ya binafsi wala ya taaluma inayoweza kukinzana na shabaha yake ya kutekeleza mchakato.

Hearing officers perform the following duties:	Maafisa wa usikilizwaji wanatekeleza majukumu yafuatayo:
• Listen to the presentation of relevant viewpoints about the due process complaint, examine all information relevant to the issues and seek to reach a timely resolution of the due process complaint; and • Provide a record of the proceedings at the cost of the state, including a written decision.	• Kusikiliza uwasilishaji wa maoni muhimu kuhusu malalamishi ya mchakato unaofaa, kuchunguza taarifa muhimu kwa matatizo na kutaka kupata suluhisho la mapema la malalamishi ya mchakato unaofaa; na • Kutoa rekodi ya kesi kwa gharama ya jimbo, ikiwa ni pamoja na uamuzi wa maandishi.
Under Part C, you are given the rights listed below in any impartial due process hearing carried out under these procedures:	Kwa mujibu wa Sehemu ya C, unapewa haki zilizoordheshwa hapa chini katika usikilizwaji wowote wa mchakato unaofaa usioegemea upande wowote unaoendeshwa kwa mujibu wa taratibu hizi:
• To be accompanied and advised by counsel and by individuals with special knowledge or training about early intervention services. • To present evidence and confront, cross examine and to compel (require) the attendance of witnesses. • To prohibit the introduction of any evidence at the hearing that has not been disclosed to you at least five (5) calendar days before the hearing. • To obtain a written or electronic word by word transcription of the hearing at no cost to you; and • To receive a written copy of the findings of fact and decisions also at no cost to you.	• Kuandamana na kushauriwa na baraza na watu binafsi walio na maarifa au mafunzo maalum kuhusu huduma za mikakati ya mapema. • Kutoa ushahidi na kukabili, kuhoji na kushurutisha (kuhitaji) mahudhurio ya mashahidi. • Kupiga marufuku uletaji wa ushahidi wowote kwenye kesi ambao hujapewa siku zisizopungua tano (5) kabla ya kesi. • Kupata unukuzi wa neno kwa neno katika maandishi au elektroniki wa kesi bila malipo kwako; na • Kupokea nakala ya maandishi ya matokeo ya ukweli na maamuzi pia bila malipo kwako.
The due process hearing (or any related activities) described in these procedures must be carried out at a time and place that is reasonably convenient to you. No later than thirty (30) calendar days after	Usikilizwaji wa mchakato unaofaa (au shughuli yoyote husika) ulioelezwa katika taratibu hizi lazima ufanywe wakati na mahali panapokufaa. Si baada ya siku thelathini (30) baada ya KDHE kupokea

KDHE receives your complaint. The due process hearing must be completed, and a written decision must be mailed to each of the parties. At the request of either party, a hearing officer may grant specific extensions beyond the thirty (30) day timeline. Any party not satisfied with the findings and decision of the due process hearing has the right to bring a civil action in state or federal court.	malalamishi yako. Lazima usikilizwaji wa mchakato unaofaa ukamilishwe na lazima uamuzi wa maandishi utumwe kwa kila mhusika. Kwa ombi la mhusika yeyote, afisa wa usikilizwaji anaweza kutoa nyongeza ya muda mahususi zaidi ya siku thelathini (30). Mhusika yeyote aliyedhulumiwa matokeo na maamuzi ya usikilizaji wa mchakato unaofaa ana haki ya kuwasilisha hatua ya umma katika mahakama ya serikali kuu.
Page 29	Page 29
During the time period of any proceeding involving a complaint, unless the Local Program and you otherwise agree, your child and family will continue to receive the early intervention services consented to on the IFSP.	Wakati wa kipindi cha kesi yoyote inayohusisha malalamishi, isipokuwa wewe na Programu ya Ndani mkubaliane vinginevyo, mtoto na familia yako wataendelea kupokea huduma za mikakati ya mapema zilizokubaliwa kwenye IFSP.
If the complaint involves an application for initial services, your child and family must be provided those services that are not in dispute.	Ikiwa malalamishi yanahusisha ombi la huduma za mwanzo, lazima mtoto na familia yako wapewe huduma hizo ambazo hazina pingamizi.
Page 30	Page 30
If you need more information about your rights (procedural safeguards) contact your local Coordinator or Kansas Early Childhood Developmental Services.	Ikiwa unahitaji maelezo zaidi kuhusu haki zako (ulinzi wa haki) wasiliana na Mratibu wako wa ndani au Kansas Early Childhood Developmental Services.
For more information, or to file an informal complaint, formal complaint or request mediation: Kansas Early Childhood Developmental Services (KECDS) Kansas Department of Health and Environment 1000 SW Jackson, Suite 220 Topeka, Kansas 66612-1274 Phone – (785) 296-3319 FAX – (785) 559-4239 KDHE.KECDS@ks.gov Parent Helpline – 1-800-CHILDREN	Kwa maelezo zaidi, au kuwasilisha malalamishi yasiyo rasmi, malalamishi rasmi au kuomba mapatano: Kansas Early Childhood Developmental Services (KECDS) Kansas Department of Health and Environment 1000 SW Jackson, Suite 220 Topeka, Kansas 66612-1274 Simu – (785) 296-3319 FAKSI – (785) 559-4239 KDHE.KECDS@ks.gov

	Simu ya Usaidizi kwa Mzazi – 1-800-CHILDREN
Advocacy Resource at: Families Together, Inc. Parent Training and Information Center(PTI): Topeka (800) 264-6343 Wichita (888) 815-6364 Garden City (888) 820-6364 famieliestogetherinc.org/	Huduma za Utetezi kwenye: Families Together, Inc. Kituo cha Mafunzo na Taarifa kwa Wazazi (Parent Training and Information Center, PTI) Topeka (800) 264-6343 Wichita (888) 815-6364 Garden City (888) 820-6364 famieliestogetherinc.org/
Due Process Hearing request must be sent to: Attn: Part C Coordinator KDHE-Kansas Early Childhood Developmental Services 1000 SW Jackson, Suite 220 Topeka, Kansas 66612-1274	Lazima ombi la Usikilizwaji wa Mchakato Unaofaa litimwe kwa: Attn: Part C Coordinator KDHE-Kansas Early Childhood Developmental Services 1000 SW Jackson, Suite 220 Topeka, Kansas 66612-1274